

Neno **mpito** maana yake ni mchakato wa mabadiliko au kubadilika kutoka hali moja au mbinu kwenda nyingine.

Mpango wa ruzuku wa pembejeo za kilimo (FISPs) ni muhimu uondolewe na kuchukuliwa na utaratibu unaopendelea kilimo ekolojia, uwekezaji wa umma katika huduma za ugani ambazo zinasaidia kilimo ekolojia, tafiti zinazomlenga mkulima na maendeleo, kuunga mkono na kutambua mfumo wa mbegu unaosimamiwa na wakulima na kuimarisha miundo mbinu (maji na barabara) – vyote ambavyo hutoa manufaa ya jumla ya muda mrefu.

Kuunga mkono mipango shirikishi

- ▶ Wakulima na maofisa ugani wa sekta ya umma wanahitaji kuungwa mkono kupitia mafunzo katika maswala ya kiufundi ya kilimo ekolojia.
- ▶ Kuna haja ya kuwa na ubia wa taaluma mbalimbali zinazovuka nyanja za kijamii, mashirika na kiufundi.
- ▶ Ni lazima kuwe na mielekeo mbalimbali ya mtiririko wa maarifa kati ya wakulima, wanasayansi, sera na mbinu, ambazo kila sehemu inaiarifu nyingine.



Kuchukua udhibiti

Wakulima wadogo ni lazima:

- ▶ wadai kujumuishwa na kushirikishwa kikamilifu katika michakato inayowaathiri;
- ▶ wafuatilie na kufanya tathmini matokeo; na
- ▶ wajipange dhidi ya njia za mchepuo wa rasilimali unaofanywa na wajanja wenye utajiri.

Kuondoa mpito wa mpango wa ruzuku ya pembejeo za kilimo